

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA LONGIDO



24 Juni, 2024

**TANGAZO KWA UMMA**

**Yah: WADAIWA SUGU WA MIKOPO YA VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU (10%)**

Halmashauri ya Wilaya ya Longido imekuwa na utaratibu wa utoaji wa mikopo kwa makundi ya Vijana, Wanawake na Watu wenye ulemavu kutoka mapato ya ndani (Mikopo ya asilimia 10%) kuanzia Mwaka Fedha 2014 hadi 2022 Mikopo iliotolewa ilipaswa kulipwa ndani ya muda husika kulingana na mikataba ya kila vikundi.

Kufuatia hali ya marejesho yasiyo ridhisha na usugu wa madeni kwa baadhi ya vikundi vilivyopewa mikopo, Halmashauri inawatangazia vikundi vyote vinavyodaiwa mikopo ambao Majina ya vikundi na wanachama yamechapishwa na kubandikwa katika mbao za matangazo za (Vijiji, Kata, Tarafa na Wilaya), website ya Halmashauri na mitandao ya kijamii.

Vikundi hivyo vinatakiwa kurejesha mikopo yao kwa haraka, kabla hatua za kisheria hazijachukuliwa.

Majina ya vikundi na wanachama yameambatanishwa pamoja na tangazo hili.

**NASSORO B. SHEMZIGWA,  
MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA WILAYA LONGIDO.**

